

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



Namba za Simu

Mkuu wa Shule: 0754255163

M/Mkuu: 0769048680

Patron: 0784992163

Shule ya Sekondari Sanya Juu

S.L.P 84,

Sanya Juu-Kilimanjaro

30/03/2022

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.....

S.L.P.....

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI
SANYA JUU: HALMASHAURI YA SIHA
MKOA WA KILIMANJARO, MWAKA 2022

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka **2022**, tahasusi ya.Shule ya Sekondari **SANYA JUU** ipo umbali wa Kilometa 50 Kaskazini-Magharibi mwa mji wa **MOSHI**. Usafiri wa basi kutoka mjini **MOSHI** unapatikana katika kituo cha mabasi **MOSHI MJINI** nauli ni shilingi za kitanzania 2000/=.

Ukitokea Arusha unashuka eneo linaitwa BOMANG'OMBE na kupanda magari ya **SANYA JUU** kwa nauli ya Tshs 1000/= . Shuka kituo kinaitwa **SANYA DAY**.

Muhula wa masomo unaanza tarehe..... Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe.....Mwisho wa kuripoti ni tarehe.....

2. Mambo Muhimu ya Kuzingatia

a) Sare ya shule yetu ni:

- i. Suruali nyeusi mbili zisizobana miguu (zisiwe model), ziwe na upana wa “inch17” kwenye miguu, mifuko mitatu isiyo na zipu,
- ii. Mashati meupe mawili ya mikono mirefu yasiyo na urembo wowote na yasiyobana mwili.
- iii. T-shirt ya shule (Itapatikana shuleni kwa gharama ya Tshs 15,000/=)
- iv. Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi.
- v. Soksi jozi mbili nyeusi
- vi. Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi isiyo na bakolu kubwa au zenye urembo.
- vii. Sweta moja rangi ya bluu nyeusi (Dark blue) liwe na shingo ya V.
- viii. Nguo za kushindia (shamba dress) ni truck suit rangiya light blue na T-shirt ya rangi ya light blue isiyo namaandishi
- ix. Tai moja rangi nyeusi,

b) Sare ya michezo kwa shule hii ni Bukta moja rangi ya bluu na T-shirt moja rangi ya bluu (sare hizi zitavaliwa wakati wa michezo tu).

2.2 Ada na Michango ya shule

a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi za kitanzania 70,000/=, Unaweza kulipa shilingi 35,000/= kwa mhula wa kwanza na kumalizia kiasi kinachobaki mhula wa pili au unaweza kulipa kiasi chote kwa pamoja.

b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni

- i. Shilingi15,000/=kwamwakakwaajiliyaukarabatiwasamani
- ii. Shilingi6,000/=kwaajiliyakitambulishonapicha
- iii. Shilingi20,000/=kwamwakakwaajiliyataaluma
- iv. Shilingi30,000/=kwamwakakwaajiliyakuwalipawapishi, walinzinavibaruawengine
- v. Shilingi 2,000/= nemboyashule
- vi. Shilingi 15,000/= kwa mwaka kwaajili ya huduma ya kwanza Tshs. 9,000/= na Bima ya Afya Tshs. 6,000/= (Wanafunzi wanashauriwa kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya CHF kikaya), Mwanafunzi mwenye Bima ya afya atalipa Ths. 9,000/= kwaajili ya huduma ya kwanza

vii. Shilingi 25,000/= Mitihani ya kujipima *mock*

viii. Fedha ya tahadhari Tshs 5000/ =(haitarejeshwa)

Jumla ya ada na michango kwa mwanafunzi ni: shilingi **188, 000/=**

Fedha zote zilipwe kwenye Akaunti ya shule **Na 40101200100**. Katika Benki ya NMB. Jina la akaunti ni *Sanya Juu Secondary School*

N.B: Malipo ya ada na michango yalipwe kwenye “pay in slip” tofauti **YASICHANGANYWE** (*Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip*)

c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

- (i) Ream mbili za karatasi kwa mwaka (plain paper 1 na nyingine ruled paper 1)
- (ii) Orodha ya Vitabu vya masomo ya tahasusi husika imeambatishwa.
- (iii) Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia
- (iv) Scientific calculator
- (v) Godoro (mzazi ana hiyari ya kununua na kuja nalo au kukodisha shuleni kwa Shilingi 10,000/= kwa mwaka)
- (vi) Mashuka pair 2 rangi ya light blue, blanketi **1**, foronya **1** rangi ya light blue, na chandarua rangiya light blue.
- (vii) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na Kikombe)
- (viii) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko
- (ix) Jembe jipya **1** na mpini wake, squeezer/mopa **1** na hard broom **1**.

3. Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule.

- (i) Wizi
- (ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
- (iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo
- (iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
- (v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
- (vi) Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
- (vii) Kufuga ndevu
- (viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
- (ix) Uvutaji wa sigara.

- (x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoia au kuolewa.
- (xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
- (xii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
- (xiii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
- (xiv) Kumiliki, kukutwa au kutumia **SIMU** ya mkononi katika mazingira ya shule
- (xv) Kudharau Bendera ya Taifa
- (xvi) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
- (xvii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

4. Viambatisho na Fomu Muhimu

- a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.
 - b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai
 - c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
 - d) Picha nne (4) (passport size) za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu
5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII



Saini ya Mkuu wa Shule...

Jina la Mkuu wa Shule: ELIETA T. KAAYA

Mhuri wa Mkuu wa Shule.....

MKUU WA SHULE
SANYAJUU SEKONDARI

TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

Mimi (mwanafunzi).....
umri.....

Jina la baba..... umri.....
Kata.....

Tarafa..... Wilaya..... Namba ya
simu..... S.L.P.....

Nani anakulipia ada
(mzazi/mlezi).....

Kama ni mlezi jina..... umri.....
Kata.....
Tarafa..... Wilaya..... Namba ya
simu..... S.L.P.....

Kiri kama utafuata sheria za shule
(mwanafunzi).....

Kiri kama utakamilisha ulipaji wa ada na michango ya shule
(mzazi/mlezi).....

Jina la mwanafunzi.....sahini.....
tarehe.....

Jina la (mzazi/mlezi).....
sahini.....tarehe.....

NB:Mwanao anapaswa kujaza fomu ya matibabu iliyoambatishwa na maelezo haya
na kuiwasilisha shuleni siku hiyo ya kuwasili.

ORODHA YA VITABU:

Kutokana na uhaba wa vitabu, mzazi/mlezi anashauriwa kumnunulia mwanae vitabu vitakavyomsaidia katika rejea na mazoezi mengine kulingana na mchepuo anaosoma kwani vitabu vilivyopo havitoshelezi kila mwanafunzi kupata kitabu chake mwenyewe. Baadhi ya vitabu hivyo ni kama vifuatavyo:-

ADVANCED MATHEMATICS.

1. Advanced Level Pure Mathematics, Fourth Edition by C. J. Tranter
2. Pure Mathematics, by J.K Backhouse
3. Engineering Mathematics sixth edition by K. A. STROUD
4. Advanced Mathematics 1-review (problems & solutions)
5. Advanced Mathematics 2-review (problems & solutions)

BASIC APPLIED MATHEMATICS:

1. Additional and Applied Mathematics by J. F. TALBERT
2. Basic applied mathematics (BAM) by Respicius Kiiza and Lugano Mwanginde
3. Basic applied mathematics review questions and solutions

BIOLOGY

1. Biological science by D.J. Taylor
2. Biology for form V&VI by Nyambari Nyangwine
3. Biology Questions and answers
4. Biology for Advanced level, new understanding, 4th Edition by Gleen & Susan Toole

CHEMISTRY

1. Chemistry in action (Michael Fremantro)
2. Advanced chemistry by Michael Clugston, Rosalind Flemming
3. Comprehensive approach to advanced level CHEMISTRY questions with answers by Sedrick C. Magas, & Kira Ernest
4. Advance chemistry-review
5. Physical chemistry with General chemistry (Advanced) by Mark Daniel Hermes Daniels.

GEOGRAPHY

1. Practical Geography by Zist Kamil
2. Approach to physical geography questions by Ahmed Lubwana
3. A comprehensive approach to physical geography for secondary school by Nyambari Nyangwine
4. Geography paper two by Msabila D.T. Msabila
5. An integrated Geography by Msabila
6. Physical geography by D.T.Msabila

PHYSICS

1. Advanced level physics 7th Edition by Nelkon and Parker
2. Advanced physics by Sterv Adams and Jonathan Allday
3. Advanced physics review
4. Principle of physics by Chand

GENERALSTUDIES

1. Contemporary Approach for advanced level general studies notes (form 5 & 6)

PRESIDENT OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
SIHA DISTRICT COUNCIL

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION


To be completed by a medical officer in respect of all form ones and five who join the school

PART A: TO THE MEDICAL OFFICER

.....

STUDENT FORM NAME:

Please examine the above named person is to be admitted to secondary school education.

Signature.....  Designation..... *Headmaster*.....

Name of head of school..... *Eheta J. Kaaya* official stamp....

MKUU WA SHULE
GANYAJUU SEKONDARI

PART B: TO BE COMPLETE BY MEDICAL OFFICER

Blood corny (red and white).....

Stool examination..... T.B. test.....

Eye test..... Ears.....

Chest..... Spleen.....

Abdomen.....

Pregnancy (girls only).....

ADDITIONINFORMATION (e.g. physical defeat or impairments)

.....
.....
.....

Please certify that the above is fit to be admitted/ taken care in secondary school. Kind of care

.....

PART C: M EDICAL OFFICER CERTIFICATE

I have examined the above named person and consider that *he/she* is not physically fit joining secondary education.

Doctor's name..... signature.....

Station..... Date.....

.....

Official stamp